## 3. KIFUA KIKUU

Kifua kikuu (TB) ni ugonjwa unaosababishwa na bakteria wanaoenezwa kwa njia ya hewa. Bakteria hao hutoka kwa mtu mwenye ugonjwa huo mara anapopiga chafya au kukohoa bila kufunika mdomo au kula vyakula (mfano maziwa) visivyopikwa vikaiva vizuri. Bakteria wanaosababisha kifua kikuu hushambulia mfumo wowote wa binadamu na kusababisha kifua kikuu cha mapafu, figo, mfumo wa

**Takwimu za hivi karibuni zinaonyesha kuwa ugonjwa wa kifua kikuu umekuwa ukiongezeka nchini na nusu ya wenye ugonjwa huu wana maambukizi ya VVU**

### Nani yuko kwenye hatari zaidi ya kupata Kifua kikuu ?

- Watumiaji wa dawa za kulevya ni rahisi kupatwa na kifua kikuu kwa sababu kinga zao za mwili huwa ni za kiwango chini na huishi mazingira yasiyo na hewa safi
- Kuwa karibu na mtu aliyekwisha ambukizwa ugonjwa huo ambae bado hajaanza matibabu (baada ya wiki 1 ya matibabu anakuwa hawezi kusambaza kifua kikuu)

### Dalili za ugonjwa wa kifua kikuu

- Kikohozi cha muda mrefu (wiki mbili au zaidi) ambapo hukohoa damu na kupata maumivu ya kifua.
- Homa ya muda mrefu ambayo hupanda usiku ikiambatana na kutokwa na jasho jingi
- Kupungua uzito kusiko kawaida kunakotokana na kukosa hamu ya kula

### Zuia kifua kikuu kwa:-

- Epuka mikusanyiko kwenye maeneo yenye hewa hafifu
- Hakikisha unafunika mdomo kwa kitambaa unapokohoa au kupiga chafya
- Unapotema makohozi hakikisha unayafukia vizuri
- Mwone daktari na kuzingatia matibabu unapoona dalili zilizoainishwa

## 4. MARADHI MENGINE

Mtumiaji kushambuliwa na magonjwa kama kaswende, klamidia, kisonono na pangusa. Wale wanaojidunga dawa za kulevya pamoja na magonjwa tajwa huwa na magonjwa ya ngozi (vidonda na majipu), tetanasi, magonjwa ya mapafu na moyo au hata kiharusi.

**Kimetayarishwa na:-**

**Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya**
**8 Barabara ya Kivukoni, S.L.P. 80327,**
**11486 Dar es Salaam, Tanzania.**
**Simu+255 22 2113753,**
**Nukushi:+255 22 2113752**
**Barua Pepe: cg@dcea.go.tz**

**MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**

# DAWA ZA KULEVYA NA MAGONJWA AMBUKIZI



## DAWA ZA KULEVYA NA MAGONJWA AMBUKIZI

Matumizi ya dawa za kulevya huleta madhara mbalimbali yakiwemo maambukizi ya VVU, homa ya ini na kifua kikuu. Maambukizi ya magonjwa haya huchochewa na tabia hatarishi miongoni mwa watumiaji wa dawa za kulevya ikiwemo kushirikiana vifaa vya kujidungia, ngono zisizo salama, kuishi mazingira yenye mzunguko mdogo wa hewa na kutochunguza afya.
Tafiti zinaonesha kuwa maambukizi haya yako juu miongoni mwa watumiaji wa dawa za kulevya ambao huwa na afya dhoofu na baadhi yao hufa mapema. Watumiaji wa dawa za kulevya huweza kusambaza maambukizi hayo kwenye jamii kutokana na kuwa na mahusiano na watu wengine. Maambukizi yanayowapata zaidi watumiaji wa dawa za kulevya ni kama ifuatavyo:-

### 1. HOMA YA INI

Ni ugonjwa unaotokana na virusi ambavyo hushambulia ini na kusababisha maradhi sugu. Virusi vinavyosababisha homa ya ini viko vya aina nyingi lakini vinavyoathiri zaidi watumiaji wa dawa za kulevya ni vya aina C na kwa kiasi kidogo aina B. Virusi hivyo husambazwa kwa njia ya damu au majimaji mengine ya mwilini:-

- Kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto wakati wa kuzaliwa.
- Njia ya kujamiiana
- Kuchangia vifaa vya kujidunga, nyembe na miswaki

**Tafiti zinaonesha kuwa virusi vya homa ya ini ni hatari kuliko VVU kwa sababu vinaweza kuishi nje ya mwili wa binadamu (yaani nje ya mfumo wa damu) kwa siku saba na vikaweza kusababisha maambukizi. VVU havina uwezo wa kuishi nje ya mfumo wa damu kwa dakika moja.**
**Takwimu mbalimbali zinaonesha maambukizi ya homa ya ini kwenye jamii ya watumia dawa za kulevya iko juu kuliko maambukizi ya VVU Tanzania ni moja ya nchi zinazoongoza kwa maambukizi ya virusi vya homa ya ini barani Afrika**

### Dalili

Watu wengi huwa hawaonyeshi dalili yoyote. Kwa maana hiyo mtu anaweza kuishi na virusi hivi na kusababisha maambukizi kwa wengine bila kugundulika. Baadhi ya wanaoambukizwa virusi hivi hupata homa, ngozi na macho kugeuka njano (manjano), kubadilika kwa rangi ya mkojo (mweusi), uchovu wa mara kwa mara, kichefuchefu, kukosa hamu ya kula, kupungua uzito, kuvimba miguu, kutapika na maumivu ya tumbo. Hali hii hudumu kwa wiki kadhaa. Virusi vya homa ya ini huweza husababisha ini kuharibika kabisa au kupata saratani ya ini.

**Mtu mwenye ugonjwa wa homa ya ini ana wastani mdogo wa kuishi kuliko mwenye maambukizi VVU.**

### Utajikingaje na homa ya ini?

- Epuka ngono zembe tumia kinga wakati wote
- Usishirikiane vifaa vyote vinavyogusa majimaji ya mwili mfano sindano, nyembe, miswaki, brashi, vitana, nk
- Mwenye maambukizi ya homa ya ini apewe mapumziko ya kutosha na chakula chenye protini na wanga mwingi kuliponya ini.
- Virusi vya homa ya ini aina C ina tiba lakini mpaka sasa haina kinga.
- Watoto wapatiwe chanjo ya homa ya ini aina B
- Dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI zinasaidia kupunguza makali ya virusi vya homa ya ini
- Pima afya yako mara kwa mara na kufuata masharti ya daktari
- Usitumie vilevi kama vile pombe, sigara, ugoro, nk.

### 2. MAAMBUKIZI YA VVU

Ongezeko kubwa la maambukizi ya VVU miongoni mwa watumiaji wa dawa za kulevya linatokana na:-

- Kushirikiana dawa, sindano, mabomba na vifaa vingine vya kujidunga
- Kutosafisha vizuri vifaa vya kujidunga. Mf. kuosha na maji ya bomba
- Kufanya ngono zisizo salama. Mfano kutotumia kinga, kubakwa, kukosa fedha ya kununulia dawa za kulevya, biashara ya ngono, kufanya mapenzi kinyume cha maumbile, nk

### Utapunguzaje maambukizi ya VVU?

- Acha matumizi ya dawa za kulevya
- Tumia sindano na vifaa vingine safi na uhifadhi mahali salama
- Tumia kinga kila unapofanya ngono
- Pima afya yako mara kwa mara
- Kama una maambukizi ya VVU zingatia tiba.